# MUUNGANO WA ELITES

**102/2** **KISWAHILI** **Karatasi ya Pili**
**(Lugha)**

**Machi 2025 – Saa: 2½**

**Jina ……………………………………………………… Na.ya Usajili……….. ….Mkondo......**

**Shule……………………………………………Tarehe……….…Sahihi……………………..**

*(a) Andika jina lako, nambari yako ya usajili na mkondo katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*(b) Andika shule, tarehe kisha tia sahihi yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*(c) Jibu maswali **yote.***
*(d) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
*(e) Majibu yote **sharti** yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
*(f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*
*(g) **Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa.***
*(h) **Watahiniwa lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo**.*

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| **Jumla** | **80** | |

1. **UFAHAMU (Alama 15)**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Mabibi na mabwana, ndugu wapenzi, alianza Bi. Mkesha, "huu ni mwaka wa tano tangu tufanye uchaguzi mkuu uliowapa vigoda wenzetu hawa. Katika kipindi hiki kumetokea mengi ya kujipigia kidari, pametokea pia mengi, mengi mabaya ya kuitia jamii ya Tungama izara Tumejipa mkono wa tahania kwa uteuzi wetu mzuri. Vilevile tumeiisuta kwa uteuzi usio wa kuridhisha

Ndugu wapenzi, sina haja ya kuwakumbusha yote ambayo tumepitia; mmeyashuhudia yote. Ila ninayotaka kusema ni kwamba malengo yetu ya kuwateua viongozi yamesalitiwa. Ndugu zangu, itakumbukwa kwamba watangulizi wetu walianza safari ya kurejesha utu wa Mwafrika wakiwa na nia thabiti ya kuwabwaga maadui watatu wa maendeleo. Je, mnawajua maadui hao? Ni ujinga, magonjwa na umaskini. Waanzilishi wa taifa hili, pamoja na viongozi waliowafuata walipigania huduma za bure za afya, na elimu ya bure na ya lazima kwa wote. Vijana wetu walijitoma ugani kuzamia lulu ya elimu; wakavidhihaki vitabu hadi kufikia kilelecha cha elimu. La kusikitisha ni kwamba elimu hii imekuwa laana kwao. Mnajua kisa na maana ya hali hii? Natija iliyotarajwa haikupatikana. Na haya si mageni kwetu. Mnajua wapo vijana humu vijijini ambao wamepiga lami kwa miaka na mikaka bila kuambulia kazi za hadhi ambazo waliahidiwa huko vyuoni. Hatimaye hawa hawa wenye shahada mbili, na wengine hata tatu, ndio wanaokuwa matarishi wa wale ambao walichechemea masomoni. Vijana wengine, kwa kukosa hata huo utarishi, wameamua kuanzisha biashara rejareja ili kujikimu; wamekosa la mama, wanaamwa la mbwa. Sina haja ya kuwafafanulia kiini cha hali hii ya kutamausha.

Ni dhahiri kwamba uthabiti wa taifa lolote lile hutegemea uthabiti wa uongozi, na uaminifu wa raia wake katika kuuwajibisha huo uongozi. Hata hivyo, inasikitisha kwamba wengi wetu tumejipoka uwezo wa kuuwajibisha uongozi kwa kuwa mawindo rahisi ya uzungukaji mbuyu. Huu ndio uwele ambao umeufisidi utu wetu na kutusahaulisha thamani za kitaifa. Hebu niambie ewe mama mwenzangu, kuna faida gani kuuza kura yako kwa kibaba cha unga na noti ya shilingi mia moja, ati kwa kuwa unaambiwa, 'Ukinichagua nitahakikisha kwamba ile Affirmative Action imezingatiwa? Ipo haja gani kuchomwa na jua ukiwafuata hawa hawa viongozi, ukiwaimbia nyimbo za kuwatia raia kichaa cha shangwe ili kuwapembeja wawapigie kura? Je,

faida kwako imekuwa gani? Hujangojea kwa kipindi chote hiki kusakafiwa kwa hiyo barabara uliyoahidiwa siku ulipouza kura yako? Na ile ahadi ya 'mwenzetu' ya kuwaajiri vijana wetu kwenye Jeshi la Wanamaii imetimia2 Hatujashuhudia watu wa akraba moja wakisombwa kutoka humu kijijini kwenda kuchukua nyadhifa katika mashirika ya umma?"

Kweli waso haya wana mji wao, Bi. Mkesha amejikosha kweliweli." Bi. Kuli alimwambia mwenzake Bi Kengemeka kisha akaendelea." Anatuambia yepi mageni ambavo masikio haya yangu yaliyokula chumvi ya miongo sita ushei ya miaka hayajasikia?

"Anasema tumpe nafasi ajitome kwenye uwanja wa majogoo," akajibu Bi. Kengemeka, "atakuwaje tofauti na hao wanaume? Hata hao wanawake tumewahi kuwapa nafasi, wakatutenda zaidi ya wanaume. Usinikumbushe kura yangu niliyoipoteza kwa kumkweza Bi. Shali kwenye usukani. Siwezi kusahau namna ile ahadi ya maji ya mabomba na kuchimbwa kwa visima ilivyoishia kwenye kauli yake tu."

Tumetendwa sote mwenzangu," alisema Bi. Kuli, inasikitisha kwamba dau la masomo ve wanangu limeenda mrama huku nikikimlilia huyo huyo Bi. Shali. Kila mara tunasikia kainitia vyombo vya habari kwamba serikali imeanzisha Hazina ya Eneobunge kuyafadhili masomo ya watoto kutoka familia maskini. Lengo kuu, nasikia, ni kuhakikisha kwamba asilimia kubwa ya watoto haipati fursa ya kujiunga na shule tu, bali pia inakamilisha masomo 'Hata hivyo, huu ni mwaka wa tatu tangu wanangu watatu waache masomo kutokana na ukosefu wa karo. Na usidhani ni karo ya shule ya kitaifa la hasha! Ni karo ya shule za kuwa ambapo niliwapeleka baada ya huyu huyu Bi Shali kunitilia huku akinitolea huko kuhusiana na ufadhili wa masomo."

"Usinikumbushe yaliyomtika mwanangu Neema," alisema Bi. Kengemeka huku akitwaa ukingo wa kanga yake kujipangusa machozi "Mwana huyu alikaa nyumbani kwa muhula nzima," akaendelea Bi. Kengemeka," dhiki ya kuwaona wenzake wakienda shuleni huku yeye anabaki nyumbani ikamfanya kuwa windo rahisi la mmoja wa hao wabunge akaambulis ambao hakuulalia wala kuuamkia. Mwenyewe mbunge ameshika hamsini zake kana kwamba hakufanya lolote. Mwanangu Jabali naye amehiari kuwa kibarua katika shamba la mbunge wa sasa. Mwenyewe anasema anataka kudunduiza pesa ili arudi shuleni kukamilisha mwaka wake wa mwisho. Na usidhani ni hao wangu tu waliofikwa na ya kuwalika. Tumewaona wana wa wenzetu

tuliopiga foleni pamoja kuwateua hao hao wabunge, wakitumiwa kama masoko ya dawa za kulevya. Wengine wamegeuzwa walanguzi wa dawa bizi." Bi. Kengemeka alikamilisha uzungumzi wake na kushusha pumzi kana kwamba ameutua mzigo mzito.

Hata hotuba ya Bi. Mkesha ilipofikia ukingoni, Bi. Kuli alimwambia mwenzake, "Ninavyoona ni kwamba wanasiasa wote wamcfinyangwa kutoka aina sawa ya udongo. Ikitokea kwamba tutampa huyu Bi. Mkesha kura, tumpe kwa kulazimika kikatiba kupiga kura, tusiwe na matarajio makuu. Inasikitisha kwamba vijana wetu waadilifu hawataki kujitia najisi kwa kuingilia siasa. Yule kijana wetu Angaza angekubali rai ya wazee kujitoma ulingoni tungemuunga mkono.

**Maswali**

a) "Malengo yetu ya kuwateua viongozi yamesalitiwa." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hoja sita kutoka kwenye taarifa. (alama 6)

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

b) Eleza mchango wa wanyonge katika hali ya uongozi nchini Tungama. (alama 3)

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………..

c) Bainisha mbinu nne ambazo Bi. Mkesha anatumia kuishawishi hadhira yake. (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………..

d)

i) Andika kisawe cha, 'kuwapembeja' kwa mujibu wa taarifa. (alama 1)

……………………………………………………………………………….

ii) Andika maana ya, 'amejikosha' kulingana na taarifa. (alama 1)

………………………………………………………………………………

***2. UFUPISHO***

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Kenya inakumbwa na hali ya hatari kuwahi kutokea msimu wa mvua ambayo imefanya serikali kuchukua hatua madhubuti za kuzuia maafa zaidi. Baada ya tathmini ya kina kuhusu hali ya hewa inayotarajiwa, serikali imelazimika kutangaza hatua za kuepusha vifo na uharibifu huku mvua ikitabiriwa kuendelea kunyesha na kimbunga kutarajiwa kutua Kenya kwa mara ya kwanza katika historia. Kimbunga hicho kitasababisha mvua kubwa, upepo mkali na mawimbi yenye nguvu na hatari, ambayo yanaweza kutatiza shughuli katika Bahari ya Hindi na makazi yaliyo karibu na pwani ya Kenya. Hali hii imechangiwa pakubwa na mabadiliko ya tabianchi.

Matukio ya hivi majuzi yamepima ustahimilivu wa nchi yetu wakati wa changamoto ambazo hazijawahi kutokea. Mvua imeendelea kusababisha mafuriko ambayo yameharibu miundomsingi. Vilevile, shughuli za uchukuzi zimetatizika katika sehemu zote za nchi baada ya barabara kuharibiwa na madaraja kusombwa na mafuriko.

Viwango vya maji katika mabwawa makuu ya ‘Seven Forks’ vimefikia kimo cha kihistoria huku mabwawa hayo yakitishia wanaoishi karibu na maeneo hayo. Kuna mabwawa 178 na vidimbwi vya

maji katika ardhi ya umma na ya kibinafsi katika kaunti 33 ambayo yamejaa na kuwa hatari kwa wakazi walio maeneo yaliyo karibu. Vifo vya watu, kufurushwa kwa watu kutoka makwao na uharibifu wa mali umeshuhudiwa nchini.

Hatari nyingine imetokana na maporomoko ya ardhi na matope katika baadhi ya kaunti na wakazi wanaoishi katika maeneo hayo watahamishwa huku wanaoishi katika maeneo yasiyoratibiwa kama ya makazi kwa mfano kando ya mito, wakipewa ilani kuhama kwa kutambua hatari iliyopo.

Kwa sababu ya janga la mafuriko, wizara ya Elimu imeagiza kuahirishwa kwa tarehe ya kufunguliwa kwa shule zote nchini kwa muhula wa pili kwa muda usiojulikana. Pia, madhara ya mvua katika baadhi ya shule ni mabaya zaidi kiasi kwamba maisha ya wanafunzi yamo hatarini. Hatua ya kuahirisha ufunguzi wa shule hadi tarehe isiyojulikana imeibua mgawanyiko wa kitabaka huku watoto kutoka familia maskini, wengi wao wanaosomea shule za umma, wakiendelea bila masomo wenzao kutoka familia tajiri wakisoma kidijitali. Isitoshe, bila tarehe mahususi za ufunguzi wa shule, ni vigumu kupanga masomo ya ziada wakiwa nyumbani. Hofu nyingine ni kuwa kukaa kwa muda mrefu bila kufanya chochote kunaweza kuwapelekea wanafunzi katika matumizi ya mihadarati na mimba za mapema.

Serikali imetangaza kuwa tarehe mpya za muhula wa pili kwa shule za msingi na za sekondari zitarekebishwa ili kufidia muda ambao ungepotezwa kwa kucheleweshwa kufunguliwa kwa shule. Tena, kutokana na mafunzo yaliyopatikana kufuatia janga la korona, wazazi wengi wanahimizwa kununua vifaa vya kidijitali vya kisasa ili kutumika katika masomo ya kidijitali.

Jeshi la Ulinzi la Kenya na Huduma ya Polisi zimeagizwa kutumia rasilmali, maafisa na vifaa vyao kuhakikisha wakenya wako salama. Wangeshirikiana na shirika la Huduma ya Vijana kwa Taifa na maafisa wa Utawala kushughulikia dharura ikiwemo kuokoa wote walio kwenye hatari.

Baraza la mawaziri limeagiza Wizara ya Fedha kutoa pesa za kusaidia kukabiliana na janga hili. Hata hivyo, kumekuwa na ukosefu wa uwazi katika utoaji wa fedha na hata misaada ambayo inakusudiwa kuendea walioathirika na vilevile haifikii wenye ulemavu-udanyanyifu katika mchakato mzima kuanzia kuwasilisha majina ya waathiriwa hadi ngazi ya malipo.

Idara ya utabiri wa hali ya Hewa nchini imewatahadharisha wakenya dhidi ya kuishi kando ya mito iliyofurika. Wanafunzi ambao tayari walikuwa wamefika shuleni walitakiwa kubaki shuleni na usimamizi wa shule ungewahifadhi na kuhakikisha usalama wao.

**Maswali:**

a) Huku ukirejelea aya **nne** za kwanza, eleza athari hasi za mabadiliko ya tabianchi. (Maneno 80) (alama 8)

**Matayarisho**

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

b) Fafanua masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya tano za mwisho. (maneno 70)

(alama 7)

**Matayarisho**

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

a) Kwa kutumia kigezo cha pahali pa kutamka, tofautisha sauti zifuatazo: (alama2)

i) /ch/ na /gh/

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………..

ii) /f/ na /th/

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

b) Onyesha miundo ya silabi katika neno **mchinjo** (alama 1)

.................................................................................................................................................

...............................................................................................................................................

c) Andika neno lenye muundo ufuatao. (alama 2)

i. Mofimu ya umoja, mzizi ………………………………………………………………….

ii. Nafsi, hali ya kuendelea, yambwa, mzizi(-f-), kauli ya kutendesha, kauli tenda

……………………………………………………………………………………………….

d) Tunga sentensi ukitumia kitenzi kishirirkishi kuonyesha dhana zifuatazo: (alama 2)

i) Kusisitiza

………………………………………………………………………………………………

ii) Kuendelea kwa kitendo

……………………………………………………………………………………………..…

e) Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo. (alama 4)

i. Magenge ambayo yanahangaisha wakazi wa mji wetu yatakumbana na polisi ana kwa ana. (andika kwa mazoea)

………………………………………………………………………………………………

ii. Mafundi waliojenga ukuta mzuri hawakulipwa chochote. (Geuza kuwa sentensi ambatano)

………………………………………………………………………………………………

iii. Nyimbo nyingi ziliimbwa tamashani. (tumia a-unganifu kuonyesha aina)

………………………………………………………………………………………………

iv. Mwalimu alisahihisha vitabu. Mwalimu alikuwa darasani. (unganisha kuwa sentensi moja ukianza kwa neno vitabu; tumia kiambishi cha wakati maalum unaodhihirika)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………...…

f) Changanua sentensi zifuatazo kwa kutumia kielelezo cha mstari.

i. Mama na baba walikuwa hodari . (alama 1)

………………………………………………………………………………………

ii. Waliosajiliwa juzi watafanya mtihani kesho. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………

g) Andika upya kwa kutumia kielezi cha idadi jumla badala ya cha wakati kilichotumika katika sentensi hii. (alama 2)

Wanaharakati walifika kortini sasa.

………………………………………………………………………………………

h) Tunga sentensi ya masharti inayoonyesha kwamba kitendo kimefanikiwa kutokana na kufanikiwa kwa kitendo kingine. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………...…

i) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? (alama 2)

i. Cherehani ……………………………………………………………………………….

ii. Nyasi ……………………………………………………………………………………

j) Andika kwa usemi halisi. (alama 2)

Kalala alimwita Gado na kutaka kujua jinsi alivyofaulu kununua gari kama hilo.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………..…

k) Andika kwa ukubwa. (alama 2)

Ndoo zao zilizopasuka zilikarabatiwa na fundi hodari.

…………………………………………………………………………………………………

l) Ainisha sentensi zifuatazo kimajukumu. (alama 2)

i. Uje kwangu leo saa tatu usiku. ……………………………………………

ii. Rais atafika kesho asubuhi. ………………………………………………..

m) Andika sentensi zifuatazo upya kwa kufuata maagizo.

i. Kausi anaweza kula ngómbe mzima. Kausi anaweza kula mbuzi. (Unganisha kuwa sentensi moja kwa kutumia kiunganishi cha kulinganisha) (alama 2)

……………………………………………………………………………………………

ii. Wote walifika mapema. (Tumia kiwakilishi cha nafsi huru badala ya neno lililopigwa mstari (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………

n) Andika kwa wingi. (alama 2)

Seremala aliyejenga karakana karibu na ufuo alitengeneza samani ya ubao.

………………………………………………………………………………………………........

.......................................................................................................................................................

o) Tunga sentensi moja kuonyesha matumizi yoyote mawili ya kinyota. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………..…

p) Andika maana mbili zinazojiotekeza katika sentensi hii. (alama 2)

Kimindi alisema atawapeleke kwa nyumba yake.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

q) Tunga sentensi moja ili kubainisha matumizi mawili ya kiambishi –i- (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….…..

r) Shaibu ni kwa ………………… kama vile choyo ni kwa karimu na ………………… ni kwa chomoa. (alama 2)

s) Kanusha sentensi ifuatayo. (alama 1)

Walilishwa na wakanyweshwa.

……………………………………………………………………………………………

**4. ISIMU JAMII. (Alama 10)**

"Mwenye sikio amesikia. Lazima tubadilishe mkondo wa mambo katika taifa letu. Sharti tuwe tayari kuteua viongozi… those who can fight for our rights kama wapiga kura.''

i) Taja na kuthibitisha sajili ya mazugumzo haya. (alama 1)

………………………………………………………………………………………………

ii. Eleza sifa zozote **tatu** za sajili kwenye mazungumzo haya; (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(b) Eleza dhima Kiswahili kama lugha ya Kitaifa. (alama 6)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOCHAPISHWA.**